# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

**14 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 14 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa

Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**304 MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kiasi gani Serikali inalinda haki ya kufanya kazi kwa Watumishi Wanawake wa Sekta Binafsi na zisizo rasmi wanaoachishwa kazi baada ya ujauzito.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**305 MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni ya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Shule ya Msingi Segese.

## WIZARA YA NISHATI:

**306 MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaanza kusambaza umeme kwenye Vitongoji vya Jimbo la Igunga.

**307 MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Vitongoji vyote vilivyobaki katika Wilaya ya Mvomero.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**308 MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuwatumia Wafungwa kuzalisha chakula chao wenyewe badala ya kununua.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**309 MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti udhalilishaji na ukatili kwa Wanawake unaofanywa kupitia Mitandao ya Kijamii.

**WIZARA YA KILIMO:**

**310 MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Maafisa Ugani katika kila Kijiji nchini kwa kuwa bajeti ya kilimo imeongezeka.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**311 MHESHIMIWA MOHAMMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni faida kiasi gani inapatikana katika Kiwanda cha Viwatilifu Kibaha na Je, Kiwanda hicho kimefikia malengo.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**312 MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Moshi utakamilika ikiwa ni pamoja na kuwalipa fidia wale waliopisha upanuzi.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**313 MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani kuyafanya maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika kama Kihesa Mgagao kuwa Vivutio vya Utalii.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**314 MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ipo tayari kuhuisha Sekta Binafsi na VETA ili Wanafunzi wanaopata ujuzi waweze kutambuliwa na VETA.

**WIZARA YA UJENZI:**

**315 MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Njia Nne kutoka Igawa hadi Tunduma utaanza.

**316 MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga madaraja ya juu Mto Chobe, Lyusa na Nkoma kwani upembuzi yakinifu umekamilika.

**317 MHESHIMIWA MARIAMU MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Azimio - Mtinga – Lukumbile - Songea hadi Makande kwa kiwango cha lami.

## WIZARA YA FEDHA:

**318 MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itatunga Sera ya Taifa ya Bima.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**14 MEI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**